



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

WAKALA WA USAJILI UFILESI NA UDHAMINI (RITA)



TAARIFA KWA UMMA

MAENDELEO YA ZOEZI LA UHAKIKI WA VYETI VYA KUZALIWA NA VIFO (VYA WAZAZI) KWA WAOMBAJI WA MIKOPO YA MASOMO YA ELIMU YA JUU KWA MWAKA 2022/23

UTANGULIZI

RITA ni Wakala wa Serikali ulio na jukumu la kusimamia na kuratibu Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu (Key Life Events) ambayo ni pamoa na vizazi na vifo. Sheria ya usajili wa Vizazi na Vifo sura 108 Toleo la 2002 imempa mamlaka Msajili Mkuu kuthibitisha uhalali wa Cheti cha Kuzaliali na cha kifo kulingana na kumbukumbu zilizopo katika Daftari la Msajili Mkuu.

Kwa mujibu wa utaratibu uliopo, wanafunzi wote wanaoomba mikopo ya Masomo ya Elimu ya Juu nchini wanatakiwa kuambatanisha nakala ya cheti cha Kuzaliali kilichohakikiwa na Msajili Mkuu wa Vizazi. Utaratibu huu pia unawahusisha waombaji wanaotakiwa kuambatisha cheti/ vyeti vya vifo vya wazazi. Lengo la kuhaliki ni kuhalikisha kila anayeoomba na kupata Mkopo wa masomo unaotolewa na Serikali ni yule anayestahili kutokana na vigezo viliviyowekwa.

Wakala unatoa huduma ya Uhakiki kwa njia ya **Kielektroniki** tu kuitia mifumo wa e- Huduma unaopatikana katika tovuti ya Wakala ambayo ni www.rita.go.tz

HALI YA UHAKIKI KUFIKIA TAREHE 27 SEPTEMBERA, 2022

Wakala ulianza rasmi zoezi la uhakiki tarehe 1 Juni, 2022. Mpaka sasa, jumla ya maombi ya uhakiki yaliyopokelewa ni **135,184** ambapo kati ya hayo **116,867** ni ya vyeti vya kuzaliali na **18,317** ya vyeti vya vifo. Wakala umeshahakiki jumla ya maombi **127,292** (sawa na asilimia 94) ambapo maombi **6,981** yilibainika kuwa na mapungufu.

Baadhi ya mapungufu katika maombi hayo ni :

- Taarifa za vyeti kutoronekana katika kumbukumbu za Msajili Mkuu
- Kutuma nakala zisizosomeka vizuri.
- Kutuma nakala zisizokuwa na namba ya ingizo

- Kutuma nakala ya vyeti viliviyotolewa nje ya nchi ambavyo RITA haina mamlaka ya kuvihakiki

HITIMISHO

Wakala umeimarisha huduma katika kitengo kinachoshughulikilia maombi ya uhakiki ili kuhakikisha maombi yanajibwa mara tu yanapopokelewa hiyo kuwawezesha waombaji kuendelea na taratibu nyingine za kuomba mikopo.

Natoa rai kwa wananchi kufuata taratibu na mifumo sahihi ya kutuma maombi ya huduma zetu ili kuepuka matapelii/ vishoka ambao huwapatia nyaraka zisizo halali hiyo kuwasababishia usumbufu mara nyaraka hizo zinapohitajika kwa matumizi. Wakala unaendelea kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama ili kuhalikisha vishoka hao wanabainika na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria.

Sambamba na hayo, tunaendelea kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma zatu kwa kuboresha mifumo ya Tehama hiyo kuwawezesha wananchi wengi zaidi kupata huduma kwa gharama nafuu.

Waombaji ambao wametuma maombi na hawajapokea majibu au wanaokabiliwa na changamoto nyininge yoyote wawasiliane na kituo chetu cha Huduma kwa Mteja kwa kupiga simu **bila malipo** namba **0800 117 482**

Imetolewa na:

Angela K. Anatomy

Kabidhi Wasii Mkuu/ Afisa Mtendaji Mkuu